

* Wataka polisi waondolewe > *

Mwanza. Wadau wamesema sheria ya uvuvi iwaondoe polisi kujihusisha na ukamataji mazao ya samaki wanaodaiwa kuvuliwa kinyume na taratibu kwa madai hawana utaalumu huo Walisema hayo wakati wa mkutano wa wadau Kanda ya Ziwa wa kukusanya maoni ya kuboresha rasimu za kubadilisha sheria ya uvuvi. Naye Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Luhaga Mpina alisema lengo la kubadili sheria hiyo imekuwa iki-sababisha changamoto nyingi. **(Jesse Mikofu)**



Kanisa laanzisha mfuko maalum

Same. Kanisa Katoliki Jimbo la Same mkoani Kilimanjaro, limezindua mfuko wa elimu kuwasaidia wanafunzi wenye vipaji maalumu na wanaotoka katika mazingira magumu. Askofu mstaafu wa Jimbo la Same, Jacob Koda alisema wanatarajia kupata zaidi ya Sh1 bilioni kutoka kwa wadau na kutoa fursa kwa watoto wanaotoka familia maskini. Naye mtawa Sarah Mdumi alisema kuna watoto wanaotoka mae-neo ya wafugaji wana uwezo mkubwa lakini wanakosa huduma na ada za shule. **(Fina Lyimo)**

Kwa Ufupi

* Mbuzi 450 waliokamatwa wataifishwa *

Moro wakwanza utekeleza agizo

Morogoro. Siku chache baada ya Rais John Magufuli kufanya kikao na wachimbaji wa madini na kuagiza kutengwa maeneo maalumu ya kuuzia madini hayo, Mkoa wa Morogoro tayari umepata eneo la kufanyia kazi hiyo.

Katibu tawala wa mkoa huo, Clifford Tandari alisema kwa kushirikiana na ofisi ya madini mkoa tayari wameanza kutekeleza maelekezo ya Rais.

Naye kaimu ofisa madini mkoa, Emmanuel Shija alisema tayari vyumba kwa ajili ya kazi hiyo vimepatikana na kwa sasa wanasubiri mitambo maalumu ya ukaguzi na ulinzi.

Mussa Juma, Mwananchi
mjuma@mwananchi.co.tz

Longido. Mbuzi 450 wanaodaiwa walikuwa wanasafirishwa kwenda kuuzwa nchini Kenya bila kulipiwa kodi wametaifishwa.

Thamani ya mbuzi hao ni ya zaidi ya Sh25 milioni, walikamatwa juzi usiku kijiji cha Kimokowa mpakani kwa Tanzania na Kenya wilayani Longido wakiwa wanasafirishwa.

Inakadiriwa kila wiki wastani zaidi ya mifugo 3,000 husafirishwa

kwenda nchini humo kwa magendo.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe alitangaza juzi kutaifishwa kwa mbuzi hao baada ya kuwaona walikohifadhiwa katika mnada wa kimataifa wa mifugo eneo la Namanga jirani na mpaka wa Tanzania na Kenya.

Alisema mbuzi hao watapigwa mnada na kwamba imekuwa kawaida kwa wafanyabiashara wa mifugo kupeleka Kenya mifugo bila kulipia kodi.

Naye mkurugenzi wa hal-

mashauri hiyo, Jumaa Mhina alisema Serikali inapoteza fedha nyingi kutokana na wafugaji kuwepa kulipa ushuru.

Wamiliki wa mbuzi hao, Lucas Saroni na Johnson Mbise walikiri kusafirisha mifugo hiyo kinyemela na kwamba inachangiwa na kodi kubwa ya Serikali.

"Kweli tulikuwa tunapeleka Kenya kwa bahati mbaya tukamatwa lakini shida ni kodi kubwa. kwani tunatakiwa kila mbuzi kulipa Sh9,500," alisema Saroni.

"Ili iwe fundisho kwa wengine tunaitafisha hii mifugo na itauzwa kwa mnada kwa watu wote na fedha zitakuwa za Serikali, hatawavumilia wafugaji wachache ambao Serikali imekuwa ikiwasaidia pembejeo kwa gharama nafuu huku mifugo wakiuza bila kulipa kodi!"

Frank Mwaisumbe



Hatima ya wanafunzi 4,000 bado njiapanda

Yonathan Kossam, Mwananchi
ykossam@mwananchi.co.tz